

1.0 UTANGULIZI

1.1 Jiografia ya Wilaya

Jiografia Na Muundo WA Wilaya

Wilaya ya Mpwapwa ni Miiongoni mwa Wilaya Kongwe ambayo iliundwa kabla ya Uhuru, Kipindi cha Utawala wa Kikoloni wa Muingereza mwaka **1947**, Aidha Wilaya ya Mpwapwa ni miiongoni mwa Wilaya saba (7) zinazounda Mkoa wa Dodoma. Makao makuu ya Wilaya yapo umbali wa km.120 kutoka Manispaa ya Dodoma yalipo Makao makuu ya mkoa wa Dodoma.

Wilaya ipo katika latitude $6^{\circ}00'$ na $7^{\circ}00'$ Kusini mwa mstari wa Ikweta na Longitudo $35^{\circ}45'$ na $35^{\circ}00'$ Mashariki mwa mstari wa 'Greenwich'.

Wilaya ya Mpwapwa inapakana na Wilaya ya Kongwa kwa upande wa kaskazini, Wilaya ya Chamwino kwa upande wa magharibi. Upande wa mashariki inapakana na Wilaya ya Kilosa (mkoa wa Morogoro) na Wilaya ya Iringa (mkoa wa Iringa).

Ukubwa wa eneo

Wilaya ina eneo la kilometra za mraba 7,479 sawa na (18.35%) ya eneo lote la Mkoa wa Dodoma. Eneo hili ambalo ni sawa na hekta 737,900 linatumika kwa shuguli za kilimo, ufugaji, hifadhi ya misitu na makazi kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 1**

Jedwali Na. 1: Mgawanyo wa matumizi ya ardhi

Eneo la kilimo (hekta)	Eneo la mifugo (hekta)	Eneo la pori tengefu (hekta)	Misitu ya hifadhi ya Taifa (hekta)	Misitu ya Vijiji (hekta)	Eneo la bwawa (hekta)	Shughuli zingine (makazi n.k) (hekta)
228,991	262,000	136,450	9,151	6,380	64,000	30,928
31%	35.3%	18.5%	1.2%	0.9%	8.7%	4.2%

Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)-Mpwapwa

1.2 Muundo na Maeneo ya Utawala

Wilaya imeundwa na Tarafa **04**, Kata **33**, Vijiji **113**, Vitongoji **575**, Mitaa **18**, Mamlaka ya Mji Mdogo **01**. Aidha Wilaya ina Majimbo ya Uchaguzi **02** ya Kibakwe na Mpwapwa.

Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa eneo la Kiutawala

TARAF	KATA	VIJIFI	VITONGOJI	MITAA
MPWAPWA	11	34	192	18
MIMA	4	13	77	-
KIBAKWE	10	32	169	-
RUDI	8	34	157	-
JUMLA	33	113	575	18

Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)-Mpwapwa

Mamlaka ya Mji Mdogo

Mji wa Mpwapwa umesharidhiwa kuwa mamlaka ya mji mdogo. Mwaka 2009/2010 Halmashauri imeunda Baraza la Mamlaka ya mji na kuwapatia Viongozi na wajumbe wake mafunzo illi kuiwezesha Mamlaka hii kuanza kazi zake kwa mujibu wa sheria kuanzia mwaka 2010/2011.

1.3 Idadi ya Watu

Kutokana na Sensa ya watu na makazi ya mwaka **2012** Wilaya ilikuwa na watu **305,056** Wanaume wakiwa **147,306 (48.3%)** na Wanawake **157,750 (51.7%)** na Kaya **66,316**. Aidha, kwa mwaka **2017** Wilaya

inakadiriwa kuwa na watu wapatao **338,461** kati yao Wanaume **163,437**, na Wanawake **175,024** wanaoishi katika Kaya **73,578**. Jedwali Na. 3 linafanua Kitarafa

Jedwali Na. 3: Idadi ya watu kwa tarafa

Na.	Idadi ya watu 2012					Makadirio ya Idadi ya watu 2017			
	Tarafa	KE	ME	JUMLA	KAYA	KE	ME	JUMLA	KAYA
1	Mpwapwa	58,546	54,276	112,822	24,526	64,957	60,219	125,176	27,212
2	Mima	21,133	19,715	40,848	8,880	23,447	21,874	45,321	9,852
3	Kibakwe	40,851	38,485	79,336	17,247	45,324	42,699	88,024	19,136
4	Rudi	37,220	34,830	72,050	15,663	41,296	38,644	79,940	17,378
Jumla		157,750	147,306	305,056	66,316	175,024	163,437	338,461	73,578

Chanzo: Matokeo ya Sensa ya Watu na Maendeleo ya Makazi 2012

1.4 Hali ya Ulinzi na Usalama

Kwa ujumla hali ya ulinzi na usalama katika Wilaya ni shwari, hakuna migogoro mikubwa inayohatarisha amani na usalama wa watu na mali zao. Amani tuliyonayo ni moja ya Matunda ya uongozi thabiti wa nchi yetu katika kutatua kero za Wananchi kwa Wakati. Tangu Serikali ya Awamu ya tano iingie Madarakani chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dr. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutekeleza Sera ya Serikali kutoa Elimu bure kuanzia Elimu ya Msingi hadi Elimu ya Sekondari kidato cha nne;

Imekuwa ni fursa kwa Wazazi kushiriki kuhamasisha Watoto wao kwenda Shule na hivyo kupunguza uwezekano wa baadhi ya Wazazi na Vijana wadogo kushiriki katika shughuli hatarishi ikiwemo Kuombaomba, kwa kisingizio cha kutafuta Ada ya Shule.

Aidha Serikali ya Awamu ya tano imeanza kutekeleza kwa kasi Kushughulikia Migogogro ya Ardhi mbapo kwa Upande wetu Mgogoro uliopo wa mpaka katika Kijiji cha Fufu kati ya Wilaya ayetu ya Mpwapwa na Majirani zetu Wilaya ya Chamwino unaendelea kutafutiwa Ufumbuzi kwa kazi kubwa.

Katika kuhakikisha kuwa Amani na Usalama uliopo unakuwa Endelevu, tumejipanga kuhakikisha kuwa viashiria vyta ya migogoro au uhalifu vinavyoitokeza vinadhibitiwa mapema kwa kushirikiana na viongozi wa maeneo husika. Ili kudhibiti migogoro ya wakulima na wafugaji Wilaya inao mkakati wa kutenga maeneo ya kilimo na mifugo. Zoezi hili limeshakamilika katika vijiji vyote **113** ambapo jumla ya hekta **262,000** zimetengwa kwa ajili ya mifugo. Pia tunatoa elimu kwa wafugaji kupanda malisho kwa lengo la kujipatia malisho ya kutosha kwa mifugo yao. Mgogoro baina ya Taasisi ya Taifa ya Mifugo na wananchi wa kijiji cha Kiboriani ni wa muda mrefu kwani wanakijiji huvamia maeneo ya Taasisi kwa ajili ya kilimo.

Jitihada zinaendelea kufanyika kwa kufanya mikutano mbalimbali ya kuwaelimisha wananchi wa juu ya Faida za Kutunza Mazingira ambapo Maeneo yote yenye Uharibifu Mkubwa wa Mazingira yamefikiwa na Mikutano ya Hadhara kati ya Mkuu wa Wilaya na Wananchi imefanyika Mfulilizo tangu Mwezi Oktoba, 2015.

Wilaya ina vituo **5** vya Polisi katika tarafa **3** na tarafa **1** iliyobaki wananchi kwa kushirikiana na Serikali wanaendelea na ujenzi wa kituo. Sambamba na hilo chini ya mpango wa Jeshi la Polisi wa maboresho kila kata ina Polisi Kata na wananchi wanapatiwa mafunzo juu ya ulinzi shirikishi kwa ajili ya kuzuia, kudhibiti na kupambana na uharifu katika maeneo yao. Mpaka sasa vikundi **131** vya ulinzi shirikishi vimeundwa na kupatiwa mafunzo kwa kuititia Polisi Tarafa na Polisi Kata wanaoishi kwenye maeneo yao. Utaratibu huu umesaidia kuimarisha amani na utulivu ndani ya Wilaya. Vile vile Wilaya imeendesha mafunzo ya mgambo kwa vijana wapatao **1,261** tangu mwaka **2005** baadhi ya vijana hao wameajiriwa katika makampuni mabalimbali ya ulinzi na wengine wameajiriwa na **SUMA JKT GUARD**.

2.0 SEKTA YA FEDHA

2.1 Mapato ya Ndani:

Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilipanga kukusanya mapato ya ndani kiasi cha shilingi **2,607,212,000.00**. Hadi kufikia mwezi Oktoba 2017 Halmashauri imekusanya jumla ya Shilingi **472,719,119.86** sawa na asilimia **15.5**.

Hali ya ukusanyaji wa Mapato ya ndani 2015/2016 – 2017/2018:

Mwaka	Lengo	Mapato halisi	% ya mapato
2015/2016	1,628,219,574.00	920,408,284	57
2016/2017	2,873,356,610.00	1,016,850,163.53	35
*2017/2018	2,607,212,000.00	472,719,119.86	15.5

* Mapato kuanzia Julai, 2017 hadi Oktoba,2017

2.2 Mapato Kutoka Serikali Kuu na Wafadhili

Halmashauri katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilipanga kukusanya /kupokea jumla ya Shilingi 45,995,310,225.00 kutoka mapato ya ndani, ruzuku kutoka Serikali Kuu na kutoka kwa wafadhili, hadi kufikia mwezi Oktoba,2017 Halmashauri imekusanya /imepokea jumla ya Shilingi 8,956,456,294.37 ikiwa ni sawa na asilimia 19.47

2.3 Changamoto:

Zifuatazo ni changamoto zilizojitokeza katika ukusanyaji wa mapato;

- **Ukame:** Kukosekana kwa mvua za kutosha imesababisha ukame ulioikumba sehemu kubwa ya Wilaya yetu na kusababisha uzalishaji kupungua wa mazao, samaki katika bwawa la Mtera na hivyo kuathiri ushuru wa mazao na samaki kupungua. Pia ukame umeathiri shughuli za ufugaji, hivyo kupunguza mapato yanayotokana na mifugo.
- **Kumekuwa na ugumu wa ukusanyaji wa ushuru wa madini na kuwapata wachimbaji hao kwani wengi ni wadogowadogo na hawana ofisi hivyo ni vigumu kuwapata.**
- **Upungufu wa watendaji wa vijiji na kata katika kukusanya mapato ya ndani.**

2.3.1 Utatuzi wa Changamoto

- Wilaya ilifanya mawasiliano na ofisi ya madini Mkoa Dodoma ili kupata takwimu za watu wote wanaojishughulisha na shughuli za madini katika Wilaya Yetu.
- Wananchi kupewa Elimu ya upandaji wa mazao yanayostahili ukame kama vile Mtama na uwele.
- Vibari vya ajria vimeombwa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kuajiri Watendaji kata, Aidha vibari vimetolewa na usahili umefanyika.

2.4 Usimikaji wa Mfumo wa Kielectronic

Halmashauri imeshafunga mfumo wa kielectronic (LGRCIS) kwa ajili ya kukusanya mapato.Utandazaji wa miundombinu umekamilika, sever zimewekwa, vifaa vimeshaunganishwa na mfumo unafanya kazi kwa kuanzia na makao makuu ya Halmashauri Wilaya. Aidha POS 60 zimenunuliwa, zimesambazwa na zinatumika kukusanya mapato.

3.0 HALI YA UCHUMI

3.1 Shughuli za Kiuchumi;

Karibu asilimia 90 ya wakazi wote hutegemea shughuli za kilimo cha mazao na ufgaji kama njia ya kujipatia mapato/chakula. Kilimo cha mazao ya chakula na biashara huajiri 50% ya wakazi wote , ufgaji 40%, biashara ndogondogo na uvuvi 7%, kazi za ofisini 2% na viwanda vidogovidogo 1%.

3.2 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Halmashauri ilikadiria kukusanya na kupokea jumla ya shilingi **47,005,161,225.00** kutoka katika vyando vyake vya ndani, Ruzuku ya Fidia (GPG), Ruzuku toka Serikali Kuu kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo, Miradi ya Maendeleo na mifuko mbalimbali. Makisio hayo yana ongezeko la shilingi 10,501,159,251.00 ambayo ni sawa na asilimia 22.3 kulinganisha na Bajeti ya mwaka 2016/2017 ambayo ilikuwa ni shilingi **36,504,001,974.00** .

Kiasi cha shilingi 13,304,145,815.00 kilipangwa kutumika ikiwa ni fedha za mapato ya ndani na ruzuku kutoka serikali kuu katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/2018 sawa na asilimia 25 ya bajeti nzima ya Halmashauri. Mchanganuo wa makadilio ya fedha za miradi ya maendeleo kama inavyooneshwa kwenye Jedwali hapo chini;:-

NA	CHANZO	KIASI	%
1	Halmashauri (Own Source)	1,564,327,200.00	11.76
2	Ruzuku Serikali Kuu	11,739,818,615.00	88.24
	JUMLA	13,304,145,815.00	100.00

Aidha hadi kufikia Oktoba,2017 kipindi cha robo ya pili , Halmashauri imekusanya na kupokea jumla ya **Shilingi. 1,148,986,574.51** sawa na asilimia **8.6** ya makisio ya bajeti kwenye miradi ya maendeleo.

3.3 Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo

Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imepokea kiasi cha shilingi **1,148,986,574.51** kutoka Serikali kuu na Wafadhili kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 8.6 ya makisio ya shilingi **13,304,145,815.00** zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018, hadi kufikia mwezi Oktoba, 2017. Maeneo yaliyopokea fedha ni EGPAF-Afyा, Mfuko wa Jimbo, Mfuko wa Jamii (TASAF) pamoja na Mpango wa Elimu Bure (FEP) Elimu Msingi .

3.4 Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo

Hadi kufikia mwezi Oktoba, 2017 kiasi cha shilingi **820,697,463.39** kimetumika kati ya shilingi **1,148,986,574.51** zilizopokelewa ukijumilishha fedha za nyongeza mfuko wa jimbo kiasi cha Shilingi 31,938,500 katika kipindi cha mwezi Julai hadi Oktoba 2017.

Matumizi haya ni sawa na asilimia 71 ya fedha zilizopokelewa. Aidha miradi mingi imeendelea kutekelezwa kwa kutumia fedha za mfuko wa Jimbo, Mpango wa Elimu bure (FEP) Elimu Msingi na Sekondari, Mfuko wa afya wa Pamoja (HSBF) na TASAF .

3.5 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Utekelezaji wa miradi unaendelea kwa kutumia Fedha zilizovuka mwaka 2016/2017 na zilizopokelewa kwa mwaka wa Fedha 2017/2018, hivyo miradi mingi inayoendelea kutekelezwa ni ukamilishaji wa miradi viporo kuanzia mwaka 2012/2013 na mwaka 2016 /2017

3.6 Changamoto katika Utekelezaji wa Miradi

Changamoto kubwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Oktoba, 2017 ni kama zifuatavyo:-

- Fedha kuchelewa au kuletwa kidogo tofauti na Mpango na bajeti ya Halmashauri, hivyo kusababisha kuchelewa kutekelezwa kwa shughuli kulingana na Mpango kazi.
- Ushiriki mdogo wa jamii kwenye kuchangia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa Maabara.

3.7 Utatuzi wa Changamoto

- Kuendelea kuomba Serikali kuleta fedha kulingana na Mpango kazi wa Halmashauri.
- Halmashauri kuendelea kutoa elimu kwa wananchi waweze kushiriki kikamilifu katika ukamilishaji wa miradi ya maendeleo.

4.0 FURSA NA VIVUTIO VYA UWEKEZAJI KISEKTA

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Wilaya imeazimia kuinua Pato la mwananchi kuitia Mikakati kadhaa mojawapo ikiwa ni kuweka mazingira Mazuri ya Uwekezaji ili kurahisisha Wawekezaji wa ndani na nje kuziona fursa na Vivutio vya Uwekezaji na hatimaye kuwekeza katika Sekta mbalimbali zilizopo Wilayani. Katika kufanikisha hili Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imeanza kuchukua hatua ambapo hadi kufikia Desemba, 2016 Wilaya imefikia hatua mbalimbali katika kuweka Mazingira Mazuri ya Uwekezaji;

- Imeanzisha Tovuti ya Wilaya kwa lengo la kutangaza Vivutio na Fursa za Uwekezaji katika bajeti ya mwaka **2017/2018**.
- Imeanzisha Kituo cha Uwekezaji cha Wilaya '**ONE STOP BUSINESS CENTER**'. Fedha imetolewa chini ya ufadhili wa **Local Investment Climate**.

Karibuni asilimia 90 ya wakazi wote hutegemea shughuli za Kilimo cha mazao na ufugaji kama njia ya kujipatia mapato/chakula. Kilimo cha mazao ya chakula na biashara huajiri 50% ya wakazi wote, ufugaji 40% , biashara ndogondogo na uvuvi 7% , kazi za ofisini 2% na viwanda vidogovidogo 1%

4.1 Uchimbaji wa madini

Sekta ya madini katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa bado ni change, ingawa kuna meneomengi yenye kusadikika kuwepo kwa madini aina mbalimbali ikiwemo Copper, Rubby, Sampire, jasi, Moonstone, Scapolite, Manganese, Peridot na Epidote. Kwa sasa uchimbaji wa madini aina ya Copper unafanyika katika vijiji vya Tambi, Mlembule, na Kinusi. Madini aina ya sapphire yanachimbwa katika kijiji cha Winza kilichopo kata ya Massa ambapo Serikali imetenge eneo la uchimbaji wa Madini lenye ukubwa wa km za mraba 40 na hadi sasa leseni 325 katilini 514 zimetolewa

5.0 SEKTA YA KILIMO

Wilaya ina jumla ya eneo la kilomita za mraba 7379. Eneo linalofaa kwa Kilimo ni hekta **223,000**. Mazao ya chakula yanayolimwa ni Mtama, Uwele, Mahindi, Viazi vitamu na Mpunga na Mazao ya Biashara ni Karanga, Ufuta na Alizeti. Eneo linaofaa kwa Umwagiliaji ni jumla ya Ha 4,452 ambapo eneo la Umwagiliaji lililoendelezwa ni Ha 2,495.

5.1 Uzalishaji wa zao la Korosho

Katika msimu wa Kilimo 2017/18 Halmashauri ya Wilaya imeendelea kuongeza uzalishaji wa miche ya korosho, usambazaji wa mbegu na utunzaji wa miche iliyokwisha pandwa katika misimu mingine iliyopita. Katika msimu wa 2017/18 Halmashauri kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania Jumla ya miche 480,000 ambayo itasambawza kwenye vijiji 17 vinavyoendeleza zao la Korosho ambavyo ni Mazae, Berege, Chitemo, Chinyika, Lukole, Kingiti, Iyenge, Nghambi, Kibakwe, Ikuyu, Pwaga, Ilolo, Pwaga, Kisokwe, Kazania, Kimagai na Idilo.

5.2 Hali ya mvua

Wilaya inapata mvua za wastani wa milimita 400-600 ambazo hunyesha kuanzia mwezi Novemba hadi mwezi Aprili ambazo hunyesha kwa wastani wa siku 60 kwa mwaka. Pia mvua hizi huwa na mtawanyiko hafifu ambao husababisha baadhi ya mazao yenye mahitaji makubwa ya maji kutostawi vizuri.

Jedwali na 2. Mwenendo wa mvua kuanzia 2014/15 HADI 2016/17

MSIMU	KUANZA	KUISHIA	SIKU ZA SIKU ZA MVUA	KIASI (MM)
2014/15	Novemba, 2014	4/4/2015	32	557.7
2015/16	Novemba, 2015	April 2016	42	848.6
2016/17	Novemba, 2016	17/04/2017	26	744.2

Chanzo: Taarifa ya Idara ya kilimo na kituo cha utafiti wa mifugo cha Taifa Mpwapwa.

5.3 Utekelezaji malengo ya kilimo 2016/17

Katika msimu wa 2016/17 jumla ya kaya 80,507 zilishiriki katika shughuli za kilimo. Jumla ya Ha **62,742** za mazao ya chakula zililimwa na kuzalisha jumla ya Tani **71,076** ikilinganishwa na malengo ya kulima Ha **79,995** za mazao ya chakula na kukadirwa kuzalisha tani **136,597**. Kwa upande wa mazao ya biashara jumla ya Ha **48,408** zililimwa na kuzalisha tani **50,923** ikilinganishwa na malengo ya kulima Ha 58,025 na kukadirwa kuzalisha tani **70,405**

JEDWALI NA. 3. MAZAO YA CHAKULA

MALENGO				UTEKELEZAJI WA MALENGO		
ZAO	HA	UZALISHAJI (T/HA)	MAKISIO MAVUNO (T)	HA	UZALISHAJI (T/HA)	MATARAJIO MAVUNO (T)
MTAMA	45,845	1.5	68,768	36,676	0.8	29,340
MAHINDI	16,384	1.5	24,576	12,228	0.6	7,337
UWELE	7,696	1.3	10,005	5,387	0.8	4,309
MPUNGA	986	2.7	2,662	887	4	3,548
MHOGO	732	4	2,928	293	3	879
VIAZI VITAMU	3,809	4	15,236	3,428	4	13,712
MAHARAGE	798	1.2	958	557	0.4	223
KUNDE	1,815	1	1,815	1,452	0.5	726
VIAZI MVIRINGO	1,930	5	9,650	1,833	6	11,001
JUMLA	79,995		136,597	62,742		71,076

JEDWALI NA.4. MAZAO YA BIASHARA

MALENGO				UTEKELEZAJI WA MALENGO		
ZAO	HA	UZALISHAJI (T/HA)	MAKISIO YA MAVUNO (T)	HA	UZALISHAJI (T/HA)	MATARAJIO YA MAVUNO (T)
KARANGA	28,760	1.3	37,388	27,322	1.2	32786
ALIZETI	18,760	1.2	22,512	16,884	0.9	15196
UFUTA	10,505	1	10,505	4,202	0.7	2941
JUMLA	58,025		70,405		48,408	50,923

5.4 UPATIKANAJI WA CHAKULA NA BEI ZAKE:

Upatikananji wa chakula ngazi ya kaya na katika masoko umeongezeka na bei za vyakula zimepungua ikilinganishwa na Mwaka 2015/16 kutohana na kuimarika kwa mazao ya chakula na biashara katika msimu wa 2016/17 . Bei za mazao zimeonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali Na.6: Bei ya mazao ya chakula katika masoko kipindi cha 2017

AINA YA ZAO	KIPIMO	BEI YA CHAKULA (SHILINGI) JANUARI 2016 – JANUARI, 2017	BEI YA CHAKULA (SHILINGI) FEBRUARI 2017–OKTOBA, 2017
Mahindi	Debe	15,000-25,000	7,000-10,000
Mtama	Debe	10,000-20,000	5,000-8,000
Maharage	Kilo	1,800-2500	1200-2500
Uwele	Debe	10,000	5,000-8000
Mcchele	Kilo	2,000-2,500	1,500-2,200
Kunde	Kilo	1,800-2,500	1,500-2,000
Ulezzi	Kilo	2,000-2500	1,800-2,500
Njugu mawe	Kilo	2500	2500-3500

Chanzo: Taarifa za masoko – Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika

5.5 MALENGO YA KILIMO MSIMU WA 2017/2018

Katika msimu wa 2017/18 imekadiriwa kulima Ha 82361 ya mazao ya chakula ambapo matarajio ni kuvuna Tani 139,597 Malengo ya mazao ya biashara ni kulima Ha 70,156, ambapo matarajio ya mavuno ni Tani 80,318 pia mazao ya bustani yamekisiwa kulimwa Ha 744 na matarajio ya mavuno ni Tani 9,688 Aidha usimamizi wa shughuli za ugani unaendelea kuimarishwa pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo ili kufikia malengo haya. Mchanganuo ni kama unavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:-

Jedwali Na 5(A) MAZAO YA CHAKULA

MALENGO			MATARAJIO
ZAO	HA	UZALISHAJI (T/HA)	MATARAJIO YA MAVUNO (T)
MTAMA	34,250	1.5	51,375
MAHINDI	23,435	1.5	35,153
UWELE	11,300	1.3	14,690
MPUNGA	886	2.7	2,392
MHOGO	1,054	4	4,216
VIAZI VITAMU	4,005	4	16,020
MAHARAGE	898	1.2	1,078
KUNDE	2,001	1	2,001
NJUGU MAWE	2,378	0.8	1,902
VIAZI MVIRINGO	2,154	5	10,770
JUMLA	82,361		139,597

B) MAZAO YA BIASHARA

MALENGO			MATARAJIO
ZAO	HA	UZALISHAJI (T/HA)	MAVUNO (T)
KARANGA	30,780	1.3	40,014
ALIZETI	25,750	1.2	30,900
UFUTA	9,404	1	9,404
KOROSHO	4,222	1.5	6,333
JUMLA	70,156		80,318

C) MAZAO YA BUSTANI

ZAO	ENEO(Ha)	T/Ha	MATARAJIO YA MAVUNO (T)
VITUNGUU	486	9	4,374
NYANYA	75	26	1,950
MCHICHA	30	20	600
MIEMBE	9	20	180
MIWA	10	30	300
KABICHI	90	20	1,800
MAHINDI MABICHI	44	11	484
Jumla	744		9,688

5.6 SHUGHULI ZINAZOTEKELEZWA ILI KUFIKIA MALENGO YA KILIMO

Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2017 shughuli mbalimbali zimeteklezwa ili kuongeza kipato pamoja na kuboresha usalama wa chakula. Aidha mkazo mkubwa umewekwa katika uendelezaji wa zao la korosho, Alizeti, mazao ya bustani na mazao yenye ufanisi mkubwa katika matumizi ya maji hususani mtama. Shughuli zilizofanyika kwa kipindi hiki ni pamoja na :-

- I. Uendelezaji wa zao la korosho ambapo uhamasishaji umefanyika kuititia :-Vikao vyta wakuu wa Idara (CMT), Kamati ya ulinzi na usalama, Baraza la biashara, Mikutano ya hadhara Vijijini

iliyoongozwa na Mkuu wa Wilaya katika Kata 20, pia uhamasishaji huu umefanyika kuitia Vyombo vyaa habari na katika kikao cha Baraza la Madiwani

- II. Uanzishaji vitalu 6 vyenye lengo la kuzalisha miche 410,000 ya korosho ambapo hadi sasa miche 320,000 imeoteshwa katika eneo la Mpwapwa mjini, Mazae, Kibakwe na Nghambi.
- III. Usambazaji wa pembejeo za zao la korosho na ukusanyaji wa takwimu katika Vijiji 17 vinavyozalisha korosho.
- IV. Kufanya kikao na maafisa ugani ili kuimarisha usimamizi katika msimu huu ili kuhimiza uandaaji wa mpango kazi na maandalizi ya msimu wa kilimo.
- V. Kutoa mafunzo ya kilimo cha mbogamboga, jinsi ya kutumia viuatilifu pamoja na masoko kwa kushirikiana na sekta binafsi TAHA katika Vijiji 6 vya Mlembule, Mafene, Kitati, Inzomvu, Tambi, Mbori.
- VI. Uendelezaji kituo cha mawasiliano na taaluma Kibakwe ambapo uchimbaji kisima kwa ajili ya mfumo wa umwagiliaji ili kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mbogamboga na uzalishaji miche ya matunda. Hadi sasa jumla ya wakulima 30 wamefundishwa ubebeshaji wa miche bora.
- VII. Kusimamia uendelezaji wa mashamba ya mihogo katika Vijiji 10 ili kupata mbegu bora katika msimu 2017/2018..
- VIII. Kutoa elimu juu ya matumizi ya zana bora za Kilimo ili kuweza kulima eneo kubwa kwa wakati na kutifua

5.7 Changamoto Zinazoikabili Sekta ya Kilimo:

Miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo ni pamoja na ;

- Upungufu wa vitendea kazi (hasa vyombo vya usafiri) kwa ajili ya kuimarisha huduma za ugani ngazi ya vijiji na kata..
- Uharibifu wa mazingira (hasa ukataji wa miti na uchomaji moto) unaosababisha ardhi yenyeye rutuba kupotea kutokana na mmomonyoko wa udongo.
- Mashamba ya wakulima hayajapimwa ili kuwawezesha kuyatumia kama dhamana ya kuombea mikopo
- Ushauri wa kitaalamu wa kulima kufuata kanda za mazao hauzingatiwi.
- Upungufu wa mvua, pamoja na mtawanyiko hafifu wa unyeshaji wa mvua
- Uwezo mdogo wa wakulima kumudu bei za pembejeo hasa zana bora za kilimo hivyo wanaendelea kutumia jembe la mkono na hivyo kusababisha tija ndogo.

5.8 Hatua zinazochukuliwa katika kukabiliana na changamoto hizi:

- Halmashauri inaendelea kutoa ushauri kwa wakulima juu ya umuhimu wa kupanda mazao kulingana na kanda za mazao na kuendeleza mazao ya viazi na mihogo
- Kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuimarisha shughuli za kilimo wakiwemo TAHA, LIC, INADES formation na wadau wa sekta binafsi wakiwemo mawakala wa usambazaji pembejeo, wasindikaji, watengenezaji zana za kilimo.
- kuwawezesha wakulima kupata taarifa na teknolojia mbali mbali katika maeneo yao.

6.0 SEKTA YA MIFUGO

Idara ya Mifugo na Uvuvi imegawanyika katika vitengo viwili; Kitengo cha Mifugo na Kitengo cha Uvuvi. Katika Wilaya ya Mpwapwa Ufugaji ni huria na wanyama wafugwao kwa kiasi kikubwa ni wa asili ambao wanakadiriwa kuwa ngombe 197,778, mbuzi 163,149, kondoo 61,977, Punda 4,710, Mbwa 14,928, Nguruwe 49,149 na kuku 204,923. Inakadiriwa kuwa mifugo inachangia karibu asilimia 45 ya pato la wilaya. Ili kutekeleza Dira ya Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa kuwa ni taasisi inayomjali mteja katika utoaji wa huduma kwa maendeleo endelevu ifikapo 2025 na Mwelekeo wetu ni kuwapatia wateja wetu huduma bora za kiuchumi, kijamii kwa kutumia misingi ya utawala bora, huduma za ugani ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii na taifa letu kiujumla kwa kuwa maafisa ugani ndio kundi pekee la wataalamu linaloshughulika na wananchi moja kwa moja.

Shughuli za Mifugo;

6.1 MIUNDO MBINU YA MIFUGO

Ubora wa mifugo ni mdogo kutokana miundombinu michache kwa ajili ya kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo. Magonjwa yanayoshambulia na kudhuru afya za mifugo na binadamu hupunguza uzalishaji na ubora wa nyama na maziwa. Ukosefu wa miundombinu unasababisha migogoro ya wakulima na wafugaji hivyo kuathiri ubora wa mifugo na mazao yake kama Nyama na Ngozi. Utoaji wa huduma za ugani kwa mifugo unategemea zaidi uwepo wa miundombinu kama majosho, vituo vya afya ya mifugo na vyanzo vya maji. Hali halisi ya miundo mbinu ya mifugo imeainishwa kwenye Jedwali Na.1

Jedwali Na.1: Hali ya miundo mbinu ya mifugo

S/N	Miundo mbinu	Hali halisi			
		Mahitaji	Iliyopo	Upungufu/ ziada	Maelezo
1	Majosho	50	28	22	24 yanafanya kazi
2	Minada	13	13	0	3 haifanyi kazi
3	Vituo vya Tiba	5	3	2	Ukarabati unahitajika
4	Krash	84	9	75	Ukarabati unahitajika
5	Machinjio	5	1	4	Yanafanya kazi
6	Majengo ya Kuanikia ngozi	8	4	4	
7	Mapakilio	4	2	3	Yanafanya kazi
8	Charcol dam	44	20	24	

Chanzo: Idara ya mifugo na Uvuvi

6.2 KUTENGA MAENEKO YA WAFUGAJI NA WAKULIMA.

Wilaya ya Mpwapwa ina eneo la ardhi lenye ukubwa wa hekta 228,991 linalofaa kwa kilimo na hekta 262,000 zinatafaa kwa ajili ya ufugaji. Katika maeneo hayo vijiji 16 vimefanyiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi na maeneo hayo yametambuliwa. Mpaka sasa Taarifa ya vijiji 7 imeshatolewa na kuonyesha eneo la Malisho ni hekta 4,035.188 na vijiji vingine taarifa inaandaliwa. Hata hivyo Vijiji ambavyo havijafanyiwa matumizi bora ya ardhi, maeneo ya malisho yanatambulika na vijiji husika.

6.3 AFYA YA MIFUGO

Idara imeendelea kukabiliana na magonjwa mbalimbali ya mifugo pamoja na kuchukua Tahadhari juu ya magonjwa ya Mlipuko. Magonjwa ambayo yanazumbua katika wilaya ni magonjwa ya Kupe (Ndigana kali, baridi, Moyo kujaa maji), Bonde la Ufa (RVF), Homa ya nguruwe, Kimeta, CBPP, CCPP, FMD, kichaa cha mbwa, Mdondo na chambavu. Magonjwa mengi yanaweza kudhibitiwa kwa kuogesha mifugo na kutoa chanjo.

6.4 HALI YA USHIRIKIANO BAINA YA TAASISI ZA MIFUGO ZA TALIRI NA LITA

Taasisi zinazoshirikiana na Idara ya Mifugo Wilayani ni LITA – Mpwapwa, Visele, Research na TVLA-Dodoma. Mahusiano yaliyopo kati ya taasisi na Halmashauri Wilaya, tukianza na LITA, wafugaji pamoja na vikundi vya wafugaji hupata mafunzo ya ufugaji bora na mifugo yao kama vile jinsi ya kufuga mbuzi wa maziwa, ng'ombe wa maziwa, kuboresha ng'ombe wa asili kwa kutumia uhimilishaji pamoja na madume bora na kuboresha kuku wa asili kwa kutumia majogooo bora.

TALIRI – kufanya tafiti mbali mbali zikiwemo za malisho ya kusambaza mbegu za malisho ndani ya Halmashauri, pia kufanya tafiti za kuboresha ng'ombe wa asili na mbuzi wa asili kwa kuwapatia wafugaji madume bora ya ng'ombe

TVLA – Mahusiano yaliyopo ni pamoja na kufanya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ya mifugo vijiji vyote vya Halmashauri wakishirikiana na wataalamu wa mifugo kutoka Ofisi ya mifugo Wilaya pamoja na wataalamu wa vijiji huisika.

SEKTA YA UVUVI

Wilaya ya Mpwapwa ni mionganini mwa Wilaya zinazonufaika na bwawa la Mtera lenye Ukubwa wa kilomita za mraba 677,660. Bwawa hili linazalisha samaki na umeme. Uzalishaji wa samaki kwa mwaka unakadiriwa kufikia tani 8,057 ambayo ni sawasawa na kilo 8,057,000 iwapo hakuna ukame

6.5 MAFANIKIO

- Afya Ya Mifugo**

Mifugo ipatayo 7,435 imepatiwa tiba na huduma mbalimbali katika kipindi cha Julay hadi September 2017 kama vile Ndigana kali, Anaemia, Kuhasi, Mapafu ya ng'ombe, Minyoo, Retained Placente, Heart water, Kuoza kwato, Kukojoa damu, Miguu na midomo, Eye infection, Ukurutu, Dystocia, CRD, Vidonda, Mapafu ya Mbuzi,, LSD, Pneumonia, Ndigana baridi, Kuharisha, Ugonjwa wa miguu na midomo, Homa ya nguruwe, Kubaki kondo la nyuma katika Vijiji/kata vya lyenge, Mpwapwa mjini, Gulwe, Mlunga, Ng'hambi, Kibakwe, Chunyu, Chamtumile, Tambi, Mlunga, Mtamba, Kidenge, Massa, Mbori, Mlimo, Mlembule, Kimagai, Mazae, Kikuyu, Lukole, Manghangu, Mlunduzi Rudi, Iwondo, Kisokwe, Ilolo, Inzomvu, Lupeta, Berege, na Ving'hawe.

- Chanjo**

Kuku wapatao 3,082 wamepatiwa chanjo ya kideri na Mbwa 1,311 chanjo ya kichaa cha mbwa katika kipindi cha Julay- September 2017 katika vijiji vya Mlunduzi, Kidenge, Mima, Ving'hawe, Inzomvu, Tambi, Mbori, Mlimo, Massa, Chunyu, Berege, na kata za Mpwapwa mjini na Massa.

- Uogeshaji**

Mifugo ipatayo 46,785 imeogeshwa katika kipindi cha Julay- September 2017 vijiji vya Kikuyu, Rudi Idilo, Berege, Mang'hangu, Mbori, Inzomvu, Kisokwe, Kimagai, , Chunyu, , , Kidenge, na Tambi.

- Kuboresha MIFUGO**

Elimu imetolewa kwa wafugaji kuboresha mifugo yao ya kienyeji na kuongeza kiwango cha maziwa na nyama kwa kutumia madume bora ya mifugo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa. Kiasi cha Madume 16, Majike 19 na majike yenye mimba 6 aina ya Mpwapwa yamenunuliwa na wafugaji katika vijiji vya Mpwapwa mjini, Lupeta, Gulwe, Vighawe, Nghambo, na Chipogoro kuanzia Julay 2016 hadi September 2017. Hii itachangia kuwa na ng'ombe wengi wenye ubora kwa kutoa maziwa kati ya lita 4 hadi 6 kwa ng'ombe wenye wastani wa kilo 250 hadi 300 ya nyama baada ya ya kupata Ng'ombe chotara

- Biashara YA MIFUGO**

Katika Wilaya ya Mpwapwa kuna jumla ya minada 13 ambayo ni Ilolo, Gulwe, Kibakwe, Rudi, Chipogoro, Mima, Msagali, Nghambi, Chogola, Mlembule (Na 30), Chitemo, Isalaza, Chisalu, na Chinyika, kati ya midada hiyo, minada 3 (Chitemo, Chisalu na Chinyika) haifanyi kazi kutokana na wafugaji kutoleta mifugo yako kwa ajili ya kuuza. Jumla ya mifugo 14,771 (Ng'ombe 3,528, Mbuzi 7,009, Kondoo 2,450, kuku 1,780 na Punda 4 yenye thamani ya Shilingi. 3,295,536,582/= wameuzwa na kusafirishwa nje ya wilaya na inakadiriwa kuipatia Halmashauri mapato ya Tsh.60,485,000/=.

- **Usajili na Utambuzi wa Mifugo**

Jumla ya Ng'ombe wapatao 37,028 wamepigwa chapa katika vijiji vya Ng'hambi,lolo, Kimagai, Lufu, Chunyu, Pandambili, Chamtumile, Ikyu, Mlembule,Makose, Chitemo, Mang'hangu, Latalawe,Berege, lyoma, Chiseyu, Gulwe, Ving'hawe, Isinghu, Nduga, Mpwapwa mjini, Igovu, Chamsisili, Seluka na Nyabu. Zoezi bado linaendelea kwa vijiji vingine.

- **Lishe**

Mradi wa utafiti wa Uimarishaji wa usalama wa chakula kupitia kuku wa kienyeji na mazao unaendelea katika kata ya lwondo. Idara ya mifugo inashirikiana na Mamlaka ya maabara ya mifugo Tanzania (TVLA) ,hata hivyo watoa chanjo wa jamii 10 dhidi ya mdondo na viongozi wa Vijii kutoka vijiji vya Igoji II na Chamanda wamepata mafunzo juu ya Ugonjwa wa Mdondo.

- **Uchinjaji, Ukaguzi na Usafi wa Nyama.**

Jumla ya Mifugo (Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo, Nguruwe, na Kuku) ipatayo 11,241 wamechinjwa na kukaguliwa katika kata za Chunyu, Lumuma, Ng'hambi, Wotta, Massa, Mpwapwa Mjini, Ving'hawe, Kimagai, Mima, Mlunduzi, Matomondo, Rudi, Chitemo, Kibakwe, Berege, lwondo, Chipogoro, Lufu, Mtera, Kingiti, Ipera, Malolo, Gulwe, Godegode, Wotta, Luhundwa, Pwaga, Rudi na Kibakwe.

- **Maonesho ya Nanenane**

Idara pamoja na wafugaji wa Ng'ombe,Kuku, Sungura,Mbuzi na Kikundi cha Ngozi(Sayuni) walishiriki maonesho ya Kilimo na mifugo –Nanenane (2017) katika uwanja wa Nzuguni Dodoma,na Mfugaji kutoka Kijiji cha Gulwe ambaye ni Ndg. Kedmond Mkwi ambaye alikuwa ni mfugaji wa ng'ombe bora wa nyama na kuzawadiwa kiasi cha Tsh 1,500,000/=Taslimu na cheti. Pia Halmashauri ilipata Cheti cha ushiriki kikamilifu.

- **Uvumi**

Wilaya Mpwapwa ni mionganoni mwa maeneo yanayonufaika na bwawa la Mtera lenye Ukubwa wa kilomita za mraba 677,660. Bwawa hili linazalisha samaki na umeme.Katika kipindi cha Katika kipindi cha Julay-September Jumla ya leseni 166 za Uvumi zimekatwa na Inakadiriwa Jumla ya Shilingi 17,563,560/= zimepatikana kutokana na ukatishaji leseni za uvumi na ushuru wa samaki.

Pia vikao cha ujirani mwema kati ya Iringa na Dodoma vinaendelea, ili Kupitia Mpango mikakati wa utunzaji wa bwawa la mtera kwa matumizi endelevu vinaendelea. Pia Moja ya mafanikio ya Kikao cha Ujirani Mwema,Katibu Tawala-Mkoa na Mkuu wa wilaya wametupatia Afisa Uvumi Kutoka Wilaya ya Chemba ambaye ameshafika na yupo kituo chake cha kazi. Katika kuhimarisha sekta ya uvumi Idara Imepata afisa Uvumi ambaye amehitimu Stashahada ya viumbe wa Majini na ameshakwenda katika kituo

cha kazi(Mtera) pamoja na afisa uvuvi mwagine ambaye anafanya kazi kwa kujitolea. Pia Elimu ya utunzaji wa bwawa na mazao yake imetolewa katika vijiji vya Chamsisiri Chibwegere na Mtera, umefanyika

- **Takwimu**

Idara imeweza kupata takwimu na taarifa za kiutendaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo, uchinjaji, magonjwa na tiba na idadi ya mifugo moja kwa moja toka ngazi ya kijiji na kata. Kwa kutumia mfumo wa utoaji wa taarifa ARDS (Agriculture Routine Data System) kata na hatimae kuunganishwa ili kupata taarifa za Wilaya za mwezi, robo mwaka na mwaka.

Fomu za kutolea taarifa hutayarishwa Wilayani na kusambazwa katika vijiji na kata. Baada ya kujazwa fomu hizo hutumwa wilayani zikiwa zimejazwa takwimu na taarifa mbalimbali zinazohitajika. Taarifa na takwimu hizi huingizwa kwenye computer ambapo mfumo wa LGMD 2i (Local Government Data Management 2i) huziunganisha takwimu hizi ili kupata taarifa za mwezi, robo mwaka na mwaka. Mfumo wa LGMD 2i ni wa kielektroniki ambapo taarifa zilizoingia huweza kuonekana na wataalam waliopo mkoani, TAMISEMI na wizara za kisekta za kilimo na mifugo kwa ajili ya mipango, sera na matumizimengine ya kisekta. Pia idara na Halmashauri kwa ujumla hutumia taarifa hizi kwa mipango na maamuzi mbalimbali kama utayarishaji wa bajeti, ujenzi wa miundombinu ya kilimo na mifugo, utoaji wa chanjo na tiba.

6.6 Changamoto

Mifugo

- Kutokupatikana dawa za ruzuku zilizotengwa na serikali.
- Ukosefu wa mvua kwa muda mrefu inayosababisha ukosefu/Upungufu wa malisho
- Upatikanaji mdogo wa Mbegu za malisho hasa African Foxtail (*Cincras ciliaris*) inayohimili ukame
- Baadhi ya wafugaji kukataa kupiga chapa mifugo yao bila sababu za msingi.

Uvuvi

- Uvuvi haramu katika Bwawa la Mtera.
- Upungufu wa maji hasa kipindi cha mvua chache husababisha wavuvi kuhama kutokana na kutokuwa na maji ya kutosha hivyo kusababisha kuhamia Manyara na Singida

6.7 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO HIZO:

Mifugo

- Idara kutenga kwenye bajeti mwaka 2017/2018 kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi
- Kuomba serikali kuleta dawa za ruzuku za kuogeshea kulingana na gawio

- Uanzishwaji / mashamba ya malisho na mashamba ya darasa ya malisho kwa ajili ya mafunzo
- Kushirikiana na Kituo cha utafiti –Mpwapwa Kuzalisha mbegu nyingi za malisho
- Kuhamasisha wafugaji kufuga mifugo yenyе tija na kuboresha mifugo yao kwa kutumia madume bora.
- Mfugaji ambaye hatapiga chapa mifugo yake, atachukuliwe hatua za kisheria kwa kutozwa faini isiyozidi milioni mbili au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja kwa mujibu wa sheria ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kifungu cha 26 cha sheria namba 12 ya mwaka 2010

Uvuvi

- Kuhimarisha vikundi vyа usimamizi shirikishi wa rasilimali ya uvuvi (BMU) katika kila Mwalo/vijiji vyа uvuvi
- Kufanya doria katika bwawa kila mara ili kudhibiti Uvuvu haramu
- Kuhakikisha wavuvi na Vyombo vyа uvuvi vinatambuliwa na kukatiwa leseni ili kuthibiti uvuvi haramu.
- Kutumia sheria mama za uvuvi na sheria ndogo za Halmashauri.
- Kuomba kibali cha kuajiri maafisa uvuvi 5
- Kuwepo mkakati wa pamoja wa wilaya tatu kuthibiti uvuvi haramu

7.0 IDARA YA ELIMU MSINGI

Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa ina shule za Msingi **117** zilizosajiliwa zenye jumla ya wanafunzi **73,248** kati yao wavulana **34,603** na wasichana **38,645**. Kati ya wanafunzi hao, jumla ya wanafunzi **64,280**, wakiwemo wavulana **30,339** na wasichana **33,941** ni wa elimu ya msingi na wanafunzi wa Elimu ya awali ni wavulana **4,264** Wasichana **4,704** wanaofanya kuwa na jumla ya wanafunzi **8,968**. Kwa upande wa walimu, Halmashauri ina jumla ya walimu **1,159** wakiwemo walimu wa darasani **1,126** na waratibu elimu kata **33**,upungufu wa walimu wa darasani ni **672**. Mahitaji ya walimu elimu ya Msingi ni **1,831**. Elimu ya Awali wanahitajika walimu **382** pamoja na madarasa yao.

7.1 HALI YA MIUNDO MBINU NA SAMANI ZA SHULE

Jedwali lifuatatalo linaonesha hali ya miundombinu ilivyo, mahitaji na upungufu uliopo.

MADARASA			NYUMBA ZA WALIMU			MADAWATI		
MAH	YAL	UPU	MAH	YAL	UPU	MAH	YAL	UPU
1,607	839	768	1,607	299	1,308	21,427	18,219	3,854

7.2 HALI YA TAALUMA

Halmashauri ya wilaya Mpwapwa imeshika nafasi ya pili kimkoa kati ya wilaya 8 zinazounda mkoa wa Dodoma kwenye mtihani wa Kuhitimu elimu ya msingi mwaka 2017. Asilimia ya ufaulu imekua ikiongezeka mwaka hadi mwaka kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini kuanzia mwaka 2014 hadi 2017.

MATOKEO YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI 2014/2017

MWAKA	WALIOFANYA			WALIOFAULU			%
	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	
2014	2,567	3,259	5,826	1,111	1,209	2,320	40
2015	2,391	3,216	5,607	1,165	1,184	2,349	42
2016	2,614	3,333	5,947	1,543	1,554	3,097	52
2017	2,344	3,165	5,509	1,746	2,150	3,896	71

7.3 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA ELIMU MSINGI

- Upungufu wa walimu unaosababisha mwalimu mmoja kuwa na vipindi vingi kwa siku, hivyo kutofundisha vyote kikamilifu na kwa ufanisi.
- Upungufu wa miundombinu hasa madarasa na nyumba za walimu

7.4 MIKAKATI YA KUINUA ALAMA ZA UFAULU

- Kuomba na kukumbusha vibari vya ajira za walimu wapya kutoka Serikali kuu
- Ujenzi na uboreshaji wa miundombinu katika shule za Elimu msingi.

8.0 DARA YA ELIMU SEKONDARI

Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa ina jumla ya shule 27 za Sekondari. Kati ya hizo 24 ni shule za Serikali, ambapo shule 04 kati ya hizo ni shule za bweni zinazota elimu ya kidato cha kwanza hadi cha sita . Shule 20 ni za kutwa za kidato cha kwanza hadi cha nne. Shule 03 ni shule zisizo za Serikali. Wanafunzi wapatao **8096** wapo shule za Serikali (wavulana **4224** na wasichana **3,872**). Shule za taasisi binafsi zina wanafunzi **245** kati yao wavulana ni **19** na wasichana **226**.

Idara ya Elimu Sekondari ina jumla ya watumishi 453 wa kada mbalimbali, kati yao Maafisaelimu waliopo ofisi ya elimu Wilaya ni 03, walimu ni 439 na watumishi wasio walimu ni 11. Pamoja na idadi hii ya walimu bado kuna upungufu wa walimu kwa masomo ya Hisabati na Sayansi.

8.1 VIFAA VYA KUFUNDISHIA, KUJIFUNZIA NA MAABARA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI

Hali ya vifaa vya kufundishia na maabara imeimarika zaidi na hivyo kufanya hali ya kujifunza na kufundisha kuimarika .Yafuatayo yamewezesha hali hii.

- Asilimia 50% ya fedha za ruzuku ya serikali katika fedha za ELIMU BURE inaelekezwa katika kuboresha upatikanaji wa vifaavya kufundishia,kujifunzia na Maabara katika shule za sekondari.
- Halmashauri ya wilaya Mpwapwa ina meza hamishika za maabara (Mobile Laboratories) sita zilizonunuliwa mwaka fedha 2014/2015 na kugawanywa katika kanda sita za shule jirani ili zitumike kwa kushirikiana. Kwa sasa meza hizo zipo katika shule za Berage,Mtera Dam, Mazae, Ipera, Kimagai na Pwaga.
- Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa ina vifaa mbalimbali kutoka shirika la maendeleo la Japan (JICA) kwaajili ya kituo cha mafunzo ya walimu kazini kwa masomo ya Sayansi na Hisabati. Vifaa hivyo ni computer, printer, Scaner, Projector, Photocopier na Duplicating machine katika shule ya Sekondari Mpwapwa.
- Maabara zilizokamili na zinatumika kwa masomo ya vitendo ni kumi na kwa shule ambazo hazijakamilisha maabara, walimu vyumba vyta madarasa na kuvitumia kama maabara kuandaa majaribio ya sayansi.

8.2 HALI YA TAALUMA

Katika taarifa hii tutajikita zaidi katika tathimini ya matokeo ya mitihani ya kitaifa kwa kidato cha Nne na Sita na kuona changamoto zinazokabili Idara na mikakati ya kutatua changamoto hizo. Mwenendo wa ufaulu kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo umoneshwa katika jedwali hapa chini;

MWENENDO WA UFAULU MTIHANI WA KIDATO CHA NNE KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU (2014-2016)

MWAKA	IDADI YA SHULE	WALIOSA-JILIWA	WALIOFANYA		WASIO NA TATIZO		WASIOFANYA		WENYE TATIZO		MATOKEO KWA MADARAJA						WALIOFAULU		WALIOSHINDWA	
			IDADI	IDADI	%	IDADI	%	IDADI	%	IDADI	%	I	II	III	IV	SIFURI	JUMLA	%	JUMLA	%
2014	26	952	928	97	804	84	24	3	124	13	18	58	110	309	309	495	62	309	38	
2015	26	1,622	1,565	96	1565	96	57	4	0	0	14	77	128	536	810	755	48	810	52	
2016	26	1,472	1,432	97	1432	97	40	3	0	0	28	40	149	620	595	837	58	595	42	
Jumla		4,046	3,925	291	3801	278	121	9	124	13	60	175	387	1,465	1,714	2,087	168	1,714	47	

8.3 HALI YA MIUNDOMBINU

Halmashauri ya Wilaya imekuwa ikiboresha miundombinu ya shule kwa kadiri fedha zilivyopatikana. Katika kipindi cha mwaka 2014, 2015- 2016 miundombinu imeendelea kuboreshwa, mfano katika shule ya sekondari MIMA kunajengwa vyumba viwili vya madarasa na vyoo matundu kumi, Shule ya sekondari Mbuga kunajengwa Nyumba ya walimu (six Mult unit), vyoo matundu kumi, na madarasa mawili, Shule ya sekondari Matomondo Nyumba ya walimu (six Mult unit) vyoo matundu kumi, na madarasa mawili. Pia Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imetekeleza ujenzi wa mabweni saba katika shule nne za kidato cha tano na sita, madarasa sita, na matundu ya vyo Hamsini na tisa kwa shule nne za kidato cha tano na sita..

Hali ya Miundombinu hadi kufikia mwezi Oktoba,2017

Na	Aina	Mahitaji	Yaliyopo	Upungufu/Ziada
1	Madarasa	260	268	6
2	Vyoo vya walimu	48	32	16
3	Vyoo vya wanafunzi	385	315	70
4	Maabara	72	10	62
5	Nyumba	372	94	278
6	Jiko	24	1	23
7	Hosteli	78	19	59
8	Maktaba	24	1	23
9	Jengola utawala	24	17	7
10	Madawati	8096	7623	473

8.4 Changamoto Zinazokabili Idara

- i. Utoro wa wanafunzi
- ii. Mimba kwa wanafunzi
- iii. Mwitiikio duni wa jamii katika suala la elimu
- iv. Upungufu wa miundombinu hasa hostel,maabara, nyumba za walimu,vyoo vya walimu na wanafunzi,
- v. Vitabu hasa vya masomo ya sanaa na lugha
- vi. Upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya ufuatiliaji
- vii. Uchakavu wa gari ya Idara za elimu
- viii. Upungufu wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati
- ix. Ukosefu wa fedha za uhamisho kwaajili ya kurekebisha ikama ya walimu

8.5 MIKAKATI

- Kuainisha mahitaji halisi ya walimu wa sayansi na kuwasilisha OWM- TAMISEMI kwa utekelezaji
- Kuhimiza wakuu wa shule na waratibu elimu kata kufanya ufuatiliaji wa ufundishaji wa mara kwa mara Maafisa ngazi ya wilaya kufanya ufuatiliaji wa ufundishaji wa mara kwa mara katika shule za sekondari
- Kutumia pesa kidogo zinazoletwa kwa kuzingatia vipaumbele

9.0 TAARIFA IDARA YA AFYA

Idara ya Afya ni mionganini mwa Idara zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa. Idara ina vitengo 2 ambavyo ni Afya Kinga na Afya Tiba. Idara ya afya ina jumla ya vituo 61 vya kutolea huduma za afya ambapo ina hospitali 1 ambayo ndio hospitali ya wilaya ,vituo vya afya 5 (Vya mashirika ya dini 2 na vya serikali 3) na zahanati 55 (Taasisi za serikali 3,Mashirika ya dini 3,Private 1 na za Umma 48)

TAARIFA YA WATUMISHI WALIOPO NA MAPUNGUFU YAKE

HOSPITALI YA WILAYA

NO	KADA	WANAOHITAJIKA	WALIOPO	UPUNGUFU
1	MADAKTARI	8	3	5
2	MADAKTARI WASAIDIZI	16	9	7
3	TABIBU	24	6	18
4	AFISA MUUGUZI	12	2	10
5	AFISA MUUGUZI MSAIDIZI	34	28	16
6	WAUGUZI WAKUNGA	41	32	9
7	WAFAMASIA	2	1	1
8	WAFAMASIA WATEKNOLOJIA	4	3	1
9	WATEKNOLOJIA MAABARA	6	2	4
10	MEDICAL RECORDER	4	0	4
11	DAKTARI WA MENO	1	0	1
12	DAKTARI WA MENO MSAIDIZI	1	0	1
12	AFISA LISHE	2	1	1
13	MTEKNOLOJIA VIFAA TIBA	2	1	1
14	KATIBU WA AFYA	1	1	0
15	DEREVA	3	1	2
16	DOBI	3	1	2

17	AFISA AFYA MAZINGIRA MSAIDIZI II	6	6	0
18	WAHUDUMU WA AFYA	68	42	26
19	WATEKNOLOJIA WASAIDIZI MAABARA	16	13	3
20	WATUMISHI WENGINEO	26	9	17
	JUMLA	280	161	129

VITUO VYA AFYA

NO.	KADA	WANAOHITAJIKA	WALIOPO	UPUNGUFU
1	MADAKTARI	4	1	3
2	MADAKTARI WASAIDIZI	4	0	4
3	TABIBU	8	2	6
4	AFISA MUUGUZI MSAIDIZI	8	4	4
5	WAUGUZI WAKUNGA	36	10	26
6	MEDICAL RECORDER	4	2	2
7	WAHUDUMU WA AFYA	32	6	26
8	AFISA AFYA MAZINGIRA MSAIDIZI II	4	4	0
9	TABIBU WA MENO	4	0	4
10	WATEKNOLOJIA WA FAMASI WASAIDIZI	4	0	4
11	WATEKNOLOJIA WA MAABARA WASAIDIZI	4	3	1
12	MADEREVA	4	4	0
	JUMLA	116	36	80

ZAHANATI

NO.	KADA	WANAOHITAJIKA	WALIOPO	UPUNGUFU
1	TABIBU	52	14	38
2	WAUGUZI WAKUNGA	104	31	73
3	TABIBU WASAIDIZI	52	8	44
4	WAHUDUMU WA AFYA	52	23	29
5	WATEKNOLOJIA WASAIDIZI-MAABARA	52	1	51
	JUMLA	312	77	235

HALI YA WATUMISHI WALIOPO NA MAPUNGUFU YAKE

NA.	KASMA	ASILIMIA YA WANAOHITAJIKA	ASILIMIA YA WALIOPO	ASILIMIA YA MAPUNGUFU
1	HOSPITALI YA WILAYA	100	58	42
2	VITU VYA AFYA	100	31	69
3	ZAHANATI	100	27	73
	JUMLA	300	116	184

TIBA

Jedwali lifuatalo hapa chini linaonyesha wagonjwa wa ndani walotibiwa kwa makundi.

I. MATIBABU YA WAGONJWA WA NDANI (IPD)

Maelezo	Umri chini ya mwezi 1		Umri mwezi 1 hadi chini ya mwaka 1		Umri mwaka 1 hadi chini ya miaka 5		Umri miaka 5 au zaidi	
	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE
Waliolazwa wodini	10	4	73	58	147	132	454	1,651
JUMLA KUU								2,529

II. MATIBABU YA WAGONJWA WA NJE (OPD)

Katika kipindi cha kuanzia Julai – Oktoba 2017 idara imetekeleza shughuli mbalimbali za kila siku.shughuli hizo zikiwa kama zilivyoainishwa hapa chini:

Maelezo	Umri chini ya mwezi 1		Umri mwezi 1 hadi umri chini ya mwaka 1		Umri mwaka 1 hadi umri chini ya miaka 5		Umri miaka 5 au zaidi		Jumla
	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	
Jumla ya Mahudhurio ya OPD	138	135	2,493	2,709	5,221	6,189	13,210	22,421	52,516
Wagonjwa waliohudhuria kwa mara ya kwanza	111	113	576	652	900	1,075	1,698	2,505	7,630
Jumla ya Mahudhurio ya Marudio	25	34	1,902	2,039	4,237	5,064	6,254	8,955	28510
JUMLA KUU	274	282	4,971	5,400	10,358	12,328	21,162	33,881	88,656

III. MAGONJWA KUMI YANAYO ONGOZA KATIKA WILAYA YETU KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI – OKTOBA 2017

NO	UGONJWA	IDADI YA WAGONJWA
1	Magonjwa ya njia ya hewa	13,793
2	Kuharisha	4,246
3	Magonjwa ya njia ya mkojo	3,245
4	Nimonia	3,145
5	Magonjwa ya ngozi	2,635
6	Magonjwa ya macho	1,606
7	Minyoo ya tumbo	1,432
8	Upasuaji	1,000
9	Magonjwa ya masikio	653
10	Malaria	458
	JUMLA	32,213

IV. HUDUMA ZA RUFAAA KWA WAGONJWA

Jumla ya rufaa 56 zilifanyika ikiwa ni wagonjwa waliotoka katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya wilayani na kuja hospitali ya wilaya kwa matibabu zaidi na jumla ya rufaa 72 zilifanyika ikiwa kupeleka wagonjwa katika hospitali ya rufaa ya mkoa kwa matibabu zaidi.

V. HUDUMA ZA ELIMU YA AFYA KWA JAMII

Huduma ya elimu ya afya kwa jamii imefanyika katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya wilayani pamoja na maeneo mbalimbali ya mikusanyiko ya watu na jumla ya watu 107,354 wamepata elimu ya afya katika wilaya yetu ikisisitiza zaidi:

- Matumizi ya kondomu
- Njia za kujikinga na ugonjwa wa malaria
- Njia za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza
- Kila kaya kujunga na bima ya afya ya jamii (CHF)

- Akina mama wajawazito wenyewe nyoka kuhakikisha wanakwenda mapema kujifungulia katika hospitali ya wilaya.
- Akina mama wajawazito ni lazima kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya.
- Kila kaya kuhakikisha inakuwa na choo bora
- Kuzingatia uzazi wa mpango

HUDUMA ZA KINGA

VI. KITENGO CHA AFYA YA UZAZI NA MTOTO JULAI-OKTOBA 2017

- Katika kitengo hiki kinashughulika na mambo yafuatayo:-
- Huduma za wajawazito
- Huduma za kujifungua
- Huduma ya kuzuia maambukizi ya virusi vya ukimwi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.
- Huduma ya uzazi wa mpango
- Huduma ya upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi.
- Huduma za chanjo kupima maendeleo ya mtoto chini ya miaka mitano na chanjo kwa akinamama
- Huduma za matibabu kwa watoto

VII. HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI NA MTOTO PAMOJA NA HUDUMA ZA UZAZI WA MPANGO

Huduma za kinga zinaendelea kufanyika katika vituo vyote vya huduma za Afya ikiwa ni pamoja na :-

1. Kliniki ya mama na mtoto pamoja na uzazi wa mpango katika vituo 55 kwa mchanganuo huu :
 - Akina mama waliohuduria clinic mahudhurio mapya - 3,228
 - Akina mama walikuja kupata huduma ya uzazi wa mpango, wateja wapya = 6,249 marudio ni 6,692

VIII. UTOAJI WA CHANJO KWA WATOTO CHINI YA MIAKA 5

NO.	AINA YA CHANJO	JUMLA YA WALIOPATA	ASILIMIA
1	BCG - Kinga inayozuia kifua kikuu	4,143	100%
2	Penta 3 – Kinga inayozuia ugonjwa wa ini na ut iwa mgongo	3,217	96%
3	Polio 3 – Kinga inayozuia kupooza kwa mwili	3,159	95%
4	PCV13 3 – Kinga inayozuia vichomi	3,359	100%
5	Rota 2 – Kinga inayozuia kuharisha	3,322	100%
6	Measles – Kinga inayozuia surua	3,095	93%

7	Tetanus TT1	2,016	60%
8	Tetanus TT2+	3,264	98%
	JUMLA KUU NI WATOTO	25,675	

IX. KITENGO CHA KIFUA KIKUU NA UKOMA

SHUGHULI ZILIZO PANGWA KUFANYIKA 2017

- Kutoa huduma sahihi kwa wagonjwa wa kifua kikuu,ukoma na wenyewe Magonjwa mawili ya kifua kikuu na Ukimwi
- Kuongeza mbini na jitihada katika kuibua wagonjwa kifua kikuu zaidi kutoka 246 kwa mwaka 2016 na kufikia 492
Kwa Wagonjwa wa Ukoma mwaka 2016 walikuwa 14, Januari- Oktoba 2017 tuna wagonjwa wa ukoma 8.
- Kutoa Elimu kazini ya jinsi ya kujikinga na kifua kikuu kwa wafanya kazi na ndugu wa wagonjwa
- Kutoa ripoti za uendeshaji shughuli za kitengo ngazi ya Mkoa na Taifa yaani Wizarani.
- Kufanya usimamizi shirikishi wa utoaji huduma katika vituo 18 vinavyotoa huduma ya kifua kikuu
- Kuimarisha mahusiano katika vituo binafsi vya afya mfano Kanisa la Roman Lumuma,Mtera Tanesco na Mt.Lukas Anglikana.
- Kuwapa ushirikiano kwa wahudumu TB ngazi ya Jamii
- Uhamasishaji kwa Jamii juu ya maambukizi ya Kifua kikuu na Ukimwi
- Elimu ya Kujikinga na Kifua kikuu mashulenii
- Ununuzi wa Shajala
- Matengenezo ya Pikipiki

X. KITENGO CHA USTAWI WA JAMII

- Kutambua wazee wasiokuwa na uwezo wa kuchangia huduma za afya ili wapate huduma hizo bure.
- Ushauri Nasaha:
- Kuunganisha wagonjwa na Ndugu zao
- Kushughulikia malalamiko ya wagonjwa
- Uhamasishaji katika uchangishaji wa damu salama

XI. MIRADI YA MAENDELEO

Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ni mionganini mwa wilaya zilizopokea fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vitu vya Afya, vituo vilivyopokea fedha na maendeleo ya ujenzi wake ni kama ifuatavyo:-

MIMA; Tumepokea kiasi cha **Shilingi 500,000,000/=** Ujenzi wa kituo hiki unafanyika kwa kutumia teknolojia ya kawaida (conventional) na Pre-fabricated. Ujenzi huu ulianza tarehe 04/12 /2017 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Januari 2018. Hatua iliyofikiwa hadi sasa. Misingi yote mitano ya nyumba, nyumba ya mtumishi, maabara, wodi ya watoto, chumba cha upasuaji na wodi ya wazazi ipo tayari pia kuta za maabara zimeshasimamishwa.

KIBAKWE; Tumepokea fedha kiasi cha **Shilingi 400,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa kituo cha Afya Kibakwe fedha hizi tumezipokea tarehe 28/12/2017.

Vilevile tunategemea kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya vya Chipogoro, Ipera na Pwaga.

Miradi mingine mbalimbali ya idara ya afya inayoendelea kutekelezwa;

- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Kisokwe ambaeo upo hatua ya lenta
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Igoji kusini ambaeo upande mmoja wa jengo umekamilika
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Chaludewa upo hatua ya umaliziaji
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Chamanda upo hatua ya umaliziaji
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Mlunduzi upo hatua ya umaliziaji
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Mzase upo hatua ya umaliziaji
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Minguwi ambaeo unaendelea
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Kitati upo hatua ya umaliziaji
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Mgoma upo hatua ya mwisho kabisa ya umaliziaji
- Ujenzi wa nyumba ya mtumishi (Two in One) katika zahanati ya Chunyu
- Ujenzi wa jengo la upasuaji katika kituo cha afya Rudi ambaeo upo hatua ya umaliziaji
- Ujenzi wa jengo la OPD katika kituo cha afya Winza ambaeo upo hatua ya umaliziaji
- Ujenzi wa jengo la OPD katika kituo cha afya Chipogoro ambaeo upo hatua ya msingi
- Ujenzi wa jengo la OPD katika kituo cha afya Mbori ambaeo upo hatua ya umaliziaji
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Singhonali ambaeo unaendelea
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Idaho ambaeo unaendelea
- Ujenzi wa nyumba ya mtumishi (Two in One) katika zahanati ya lyenge
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Malolo ambaeo unaendelea
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Itende
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Iguluwi ambayo ipo hatua ya msingi
- Ujenzi wa nyumba ya mganga katika zahanati ya Mzase
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Chiseyu ambapo jengo lipo hatua ya msingi
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya lyoma
- Ujenzi wa nyumba ya mganga katika zahanati ya Igoji kusini
- Ujenzi wa jengo la zahanati ya Kingiti

Ujenzi wa zahanati hizi ukikamilika ina maana jumla vijiji 69 vitakuwa na zahanati na juhudii za kuendelea kujenga zahanati ili kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati katika wilaya yetu zinaendelea kwa kushirikisha nguvu za wananchi.

Wilaya yetu ina kata 33 na kwa sasa tuna vituo vya afya 2 vinavyofanya kazi na vituo vingine 4 vinaendelea kujengwa katika kata za Matomondo,Mima,Chipogoro na Masa na lengo ni kuendelea kushirikisha nguvu za wananchi ili kuhakikisha kila kata inakuwa na kituo cha afya.

10.0 KITENGO CHA DAWA

RIPOTI YA MANUNUZI YA DAWA KWA ROBO MWAKA JULAI – DISEMBA-2017

Jumla ya Shilingi **189,710,325/=** zimetumika kununulia dawa na vifaa tiba ikiwa Shilingi **151,123,100/=** zilinunua dawa kutoka MSD na **Shilingi 38,587,225/=** zilitumia kununua dawa kutoka kwa mzabuni teule (Prime Vendor).

CHANGAMOTO

- Upungufu mkubwa wa watumishi wenyewe ujuzi kwani katika zahanati 17 kuna mtumishi mmoja mmoja tu hivyo kusababisha wananchi kukosa huduma mara kwa mara wakati mtumishi akienda likizo,akileta taarifa wilayani,akienda kwenye mafunzo n.k.
- Miundombinu mibovu ya barabara ambapo inasababisha kushindwa kufanya usimamizi shirkishi pamoja na kusambaza dawa na chanjo hasa kipindi cha masika katika maeneo ya Mang'aliza, Matonya, Galigali, Lufu, Iwondo, Wotta, Chinyagh'uku, Mlondizi.
- Ucheleweshwaji wa fedha za miradi ambapo husababisha miradi kujengwa kwa muda mrefu bila kukamilika
- Uchakavu mkubwa wa baadhi ya zahanati.
- Upungufu wa nyumba za watumishi.
- Madeni ya vituo kwenye akaunti ambazo zipo MSD yanayosababisha kukosekana kwa dawa kwa baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya
- Jengo la mochwari ni dogo halitoshelezi
- Friji la kuhifadhia maiti ni dogo halikidhi mahitaji pia ni chakavu.
- Baadhi ya zahanati kuwa na mtumishi mmoja mmoja hivyo kusababisha wakati mwengine kituo kufungwa pindi mtumishi huyo anapopeleka taarifa wilayani, anapokwenda semina, anapopata dharura n.k.
- Kucheleweshwa kwa fedha za mfuko wa pamoja wa afya (Health Basket Fund) ambapo husababisha shughuli zilizopangwa kuchelewa kufanyika kwa wakati.
- Fedha za OC zinakuja kidogo na haziji kwa wakati hivyo kusababisha kukosa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli kama vile ununuzi wa mafuta kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa, mafuta kwa ajili ya kuendesha jenereta la hospitali katika kipindi ambacho umeme unapokatika pia fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo ya magari hasa magari ya kusafirisha wagonjwa (Ambulance).
- Upungufu wa mafuta (diesel) kwa ajili ya kwenda kutoa huduma ya mkoba
- Kushuka kwa huduma ya akinababa kusindikiza wenza wao kliniki

MIKAKATI

- Kuendelea kuwasiliana na idara ya ujenzi waendelee kuboresha barabara ili kuhakikisha zinapitika muda wote
- Kuendelea kuomba kibali cha ajira utumishi ili kuhakikisha kila mwaka tunapata watumishi ajira mpya tukiwa na lengo la kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi
- Kununua dawa,vifaa tiba na vitendanishi nya maabara toka kwa mzabuni wa dawa kwa kutumia fedha za CHF,NHIF na Papo kwa papo ili kukabiliana na upungufu wa dawa toka Bohari kuu ya taifa ya dawa (MSD)
- Kushirikisha nguvu za wananchi ili kuhakikisha tunajenga vituo nya afya katika kila kata na zahanati katika kila kijiji pamoja na nyumba za watumishi

11.0 Taarifa ya Huduma za Maji

11.1 Watumishi wa Sekta ya Maji

Mahitaji ya Watumishi katika Sekta ya Maji (Maji Vijijini) ni 27 waliopo ni 9 Upungufu ni 18 kama inavyoonekana katika katika **Jedwali 3**. Upungufu unatokana na Watumishi 8 kustaafu kwa mujibu wa Sheria katika kipindi cha miaka 3, Watumishi 2 kufariki dunia, Watumishi 4 kuhamishiwa katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira.

Jedwali Na.3 Hali ya Watumishi

Na	Kada	Ikama	Waliopo	Pungufu
1.	Wahandisi	4	1	3
2.	Mafundi Sanifu	23	8	15
	JUMLA	27	9	18

Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)-Mpwapwa

11.2 Hali ya Utoaji wa Huduma ya Maji:

Wilaya ya Mpwapwa ina jumla ya vyanzo nya maji vипатавуо 306, ikiwemo maji ya mtiririko 32, visima virefu vipo 55, visima vifupi 145, matenki ya kuvunia maji ya mvua 43, vyanzo nya asili vilivyoboreshwa 31. Hata hivyo ni vyazo 242 ndivyo vinavyofanyakazi kama inavyoonyesha kwenye **Jedwali na 4**. Idadi ya watu wanaopata Huduma ya Maji Safi na Salama ni 121,570 sawa na asilimia 53.5 ya makadirio ya watu wapataao 323,947 katika Wilaya ya Mpwapwa. Hata hivyo Watu 90,340 katи ya watu 282,312 waishio Vijijini ndio wanaopata Huduma ya Maji Safi na Salama sawa na asilimia 32. Watu 31,250 katи ya 41,635 wanaoishi Mjini ndio wanapata huduma ya Maji Safi na Salama sawa na 75%. Huduma ya Maji Mjini inasimamiwa na Bodi ya Maji Mjini Mpwapwa iliyonzishwa mwaka 2003.

Jedwali na 4. Hali ya Vyanzo vya Maji

Na.	Aina ya chanzo	Idadi	Vinayofanya kazi	Visivyofanya kazi
1	Visima Virefu	55	37	18
2	Skimu za maji ya mtiririko	32	28	4
3	Visima vifupi vinavyotumia pampu za mkono	145	105	40
4	Matanki ya kuvunia maji ya Mvua	43	43	0
5	Vyanzo vya asili vilizoboreshwa	31	29	2
	JUMLA	306	242	64

12.00 Uboreshaji wa Huduma za Maji Vijijini

12.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maji Kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II)

Katika Kipindi cha Mwaka 2014/2015 na 2015/2016, Halmashauri imekamilisha ujenzi wa miradi 5 katika Vijiji vya Kimagai, Chunyu, Chinyang’huku, Wiyenzele na Kisima ambayo inawahudumia watu wapatao 18,145. Miradi hii imegharimu Jumla ya shilingi za Kitanzania 1,700,540,703.93 kama ilivyoonyeshwa katika **Jedwali na 5**. Hata hivyo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ilipanga kutekeleza miradi mipy 7 katika Vijiji vya Kidenge, Mzase, Iramba, Mima, lyoma, Kibakwe na Bumila. Aidha Halmashauri ilipanga kukarabati miradi 3 katika Vijiji vya Kingiti/Lukole, Chogola na Seluka kama ilivyoonyeshwa katika **Jedwali na 6**. Hata hivyo miradi hii imechelewa kutekelezwa kutokana na kuchelewa kupatikana fedha za Usanifu kutoka Serikalini. Kwa sasa Usanifu wa miradi yote umekamilika, zabununi kutangazwa na wakandarasi wameshapatikana. Aidha miradi hii inatekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018. Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza kiwango cha utoaji wa Huduma ya Maji Vijijini kutoka asilimia 32 ya sasa hadi kufikia asilimia 55.

Jedwali na. 5 Miradi iliyotekelawa 2014 - 2016

MWAKA	IDADI YA MIRADI ILIYOJENGWA	MHALI / KIJIJI	GHARAMA	IDADI YA WANAUFAIAKASI	MAELEZO
2014/2015	3	Kimagai	347,486,699.93	4168	Mradi umekamilika na unatoa huduma
		Chunyu	305,510,139.00	5492	Mradi umekamilika na unatoa huduma
		Chinyang'huku	405,273,200.00	2827	Mradi umekamilika na unatoa huduma
2015/2016	2	Wiyenzele	341,866,135.00	2079	Mradi umekamilika na unatoa huduma
		Kisima	300,404,530.00	3579	Mradi umekamilika na unatoa huduma
JUMLA			1,700,540,703.93	18,145	

Jedwali na 6 Miradi ya mwaka 2016/2017 inayotekelawa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018

S/N	JINA LA MKATABA	JINA LA MKANDARASI	MUDA WA MKATABA	GHARAMA YA MKATABA	MAELEZO
1	UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI KATIKA KIJIJI CHA IRAMBA.	BAREGEREJE CONSTRUCTION WORKS LTD., P.O BOX 2931, DODOMA.	SIKU 180	376,808,173.39	Mkataba Na.LGA/023/2016/2017/ W/18 umesiniwa tarehe 03/11/2017
2	UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI KATIKA KIJIJI CHA IYOMA.	FHS ENGINEERING LIMITED, P.O BOX 32972, DAR ES SALAAM.	SIKU 180	409,053,717.00	Mkataba Na.LGA/023/2016/2017/ W/19 umesiniwa tarehe 03/11/2017
3	UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI KATIKA	WAGERASI INVESTMENT LTD., P.O BOX	SIKU 180	478,604,719.00	Mkataba Na.LGA/023/2016/2017/ W/20 umesiniwa tarehe

	KIJIJI CHA KIBAKWE.	42704, DAR ES SALAAM.			03/11/2017
4	UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI KATIKA KIJIJI CHA BUMILA.	ADVANCED ENGINEERING CO. LTD., P.O BOX 55093, DAR ES SALAAM.	SIKU 180	513,724,958.00	Mkataba Na.LGA/023/2016/2017/ W/23 umesiniwa tarehe 03/11/2017
5	UJENZI WA MIUNDO MBINU YA MAJI KATIKA KIJIJI CHA MIMA.	JEMASON INVESTMENT CO. LTD., P.O BOX 4277, DAR ES SALAAM.	SIKU 180	428,929,937.00	Mkataba Na.LGA/023/2016/2023/ W/18 umesiniwa tarehe 03/11/2017
6	UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI KATIKA KIJIJI CHA MZASE.	DAN GENERAL CONSTRUCTION (T) LTD. of P.O.BOX 90434, DAR ES SALAAM.	SIKU 180	432,022,172.89	Mkataba Na.LGA/023/2016/2017/ W/24 umesiniwa tarehe 03/11/2017
7	UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI KATIKA KIJIJI CHA KIDENG.	MBESSO CONSTRUCTION CO. LTD., P.O BOX 79660, DAR ES SALAAM.	SIKU 180	1,070,460,729.80	Mkataba haujasainiwa
8	UCHIMBAJI WA VISIMA VIREFU KATIKA VIJIJI VYA BUMILA NA MLUNDUZI.	VICTORIA BOREHOLES DRILLING LTD., P.O BOX 1352, DAR ES SALAAM.	SIKU 90	69,363,822.00	Mkataba Na.LGA/023/2016/2017/ W/25 umesiniwa tarehe 03/11/2017
9	UKARABATI WA MIUNDOMBINU YA MAJI KATIKA KIJIJI CHA CHOGOLA.	WEBB & SON COMPANY LIMITED, P.O BOX 70792, DAR ES SALAAM.	SIKU 90	107,603,256.00	Mkataba Na.LGA/023/2016/2017/ W/26 umesiniwa tarehe 03/11/2017

10	UKARABATI WA MIUNDOMBINU YA MAJI KATIKA VIJII VYA LUKOLE NA KINGITI.	SEPRO ENGINEERING & GENERAL TRADERS LTD., P.O BOX 20862, DAR ES SALAAM.	SIKU 90	184,756,612.00	Mkataba Na.LGA/023/2016/2017/ W/18 umesiniwa tarehe 03/11/2017
11	UKARABATI WA MIUNDOMBINU YA MAJI KATIKA KIJINI CHA SELUKA.	GWANTWA CONSTRUCTION LTD., P.O BOX 15445, ARUSHA.	SIKU 90	157,543,334.00	Mkataba Na.LGA/023/2016/2017/ W/27 umesiniwa tarehe 27/10/2017
JUMLA				4,228,871,431,08	

Miradi hii ikikailika itawanufaisha wakazi wapatao 65,829.

12.2 Mkakati wa Wilaya wa kuongeza Hali ya Utoaji wa Huduma ya Maji

12.2.1 Utafiti wa maji chini ya ardhi na Uchimbaji wa visima virefu

Katika kipindi hiki cha mwaka 2017/2018 Halmashauri ilipanga kuchimba Visima virefu 16 katika Vijiji vya Mbonyuni, Ng'hambi, Kisisi, Mgoma, Munguwi, Inzomvu, Mang'hangu, Idilo, Pwaga, Chitemo, Igoji II, Mbije, Chinyika, Makose, Idodoma na Gulwe. Jumla ya Shilingi 661, 656,798 zimetengwa kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kazi hii.

12.2.2 Kufanya upembuzi yakinifu wa miradi ya maji ya mtiririko

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashuri imepanga kufanya upembuzi yakinifu (Feasibility Study) Njia Panda, Lutawale, Iguluwi, Nzugilo, Malolo, Lufusi, Mafene, Kitati, Mbuga, Tambi, Mwenzele na Mlembule (Nduga). Jumla ya Shilingi 222,404,000 zimetengwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kazi hii.

13.0 Elimu ya Uvunaji wa Mvua kwa Jamii

Halmashauri inaendelea kuhakikisha kuwa:

- Elimu juu ya uvunaji wa maji ya mvua inaendelea kutolewa kwa kuwashirikisha wadau wote
- Wilaya inakamilisha mchakato wa kutunga sheria ndogo juu ya uvunaji wa maji ya mvua
- Kutoa mafunzo kwa mafundi wa Jamii yanayohusu ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua

- Kufunga miundombinu ya mfano ya uvunaji wa maji katika baadhi ya vijiji kama sehemu ya kujifunzia
- Kujenga malambo (charcoal dam) na mabwawa vijiji ili kuongeza upatikanaji wa maji ya mvua.

14.0 Ushirikishwaji wa Wananchi

Wananchi wamekuwa wakishirikishwa katika ujenzi na Uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji. Hadi sasa kuna mifuko ya maji 70 iliyofunguliwa katika Benki za NMB na CRDB. Inakadiriwa kuwa Jumla ya Shilingi. 65,115,936.64 zipo kwenye akaunti za Mifuko ya Maji ya Vijiji inayosimamiwa na Kamati za Maji na Vyombo Huru vya Watumiaji Maji. Fedha hizi hutumika kwa shughuli za Uendeshaji na Matengenezo ya Miradi ya Vijiji.

5.1 Uundaji wa Vyombo Huru vya Watumiaji Maji (COWSO)

Halmsahuri imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maji Namba 12 ya mwaka 2009 ya uanzishaji wa Vyombo Huru vya watumiaji. Hadi sasa Jumuiya za Watumiaji 39 zimeundwa. Aidha Halmashauri imeweka Mkakati wa kuunda Vyombo Huru vya Watumiaji Maji kama ilivyoonyeshwa kwenye **Jedwali na 7**.

Jedwali na 7 COWSO zilizoundwa

Na	Vyombo Huru (COWSO) vilivyoundwa na Kusajiliwa	Lengo la COWSO zitakazo sajiliwa			Jumla
		2017/2018	2018/2019	2019/2020	
1	39	20	20	20	99

15.0 Changamoto na hatua za kukabiliana na changamoto Pamoja na mafanikio yaliyopatika zipo changamoto kama ifuatavyo;

1. Upungufu wa wataalam wa Sekta ya Maji hasa kada za Mafundi Sanifu.	1. Kuweka kwenye bajeti na kuomba kibali cha kuajiri Wataalamu wa Sekta ya Maji
2. Kuchelewa / kutoletewa kabisa fedha za utekelezaji wa miradi zilizobajetiwa katika bajeti ya mwaka wa fedha.	2. Kuendelea kufanya mawasiliano na Wizara ya Maji ili kupata ufumbuzi wa kutatua suala la upatikanaji wa fedha kwa wakati.
3. Kuchelewa kwa Uchangiaji wa gharama ya ujenzi wa miradi ya maji kutoka kwa Jamii.	3. Kuhamasisha Jamii kuchangia miradi ya maji miradi ya maji na kutunisha mifuko ya maji.
4. Mwingiliano wa majukumu baina ya Kamati za Maji, Viongozi wa Vijiji na Vyombo Huru vya Watumiaji Maji.	4. Kutoa Elimu ya Utawala Bora na Usimamizi wa Miradi ya Maji.
5. Uchakavu wa miundombinu ya maji iliyojengwa muda mrefu.	5. Kufanya ukarabati wa miradi ya maji iliyojengwa

6. Upungufu wa fedha za matengenezo madogo na ufuatiliaji wa miradi ya maji Vijijiini.	6. Kuunda na kuvijengea uwezo Vyombo Huru vya Watumiaji Maji (COWSO) ili viweze kusimamia na kuendesha miradi ya maji
7. Uelewa na tafsiri duni ya Sera ya Maji, Sheria za Maji na 11 na 12. za mwaka 2009.	7. Kutoa Elimu kwa Jamii kuhusu Utekelezaji na Usimamizi wa Sera ya Maji ya mwaka 2002, Sheria za Maji namba 11 & 12 za mwaka 2009
8. Suala la Usimamizi wa Pamoja wa Rasilimali za Maji kutopewa kipaumbele.	8. Kutoa elimu na Mafunzo ya Usimamizi wa Pamoja wa Rasilimali za Maji.

16.0 Uboreshaji wa Huduma za Maji Mjini.

Mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji mjini Mpwapwa kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (FDA) umekamilika kwa 100%. Jumla ya watu 31,250 kati ya 41,635 wanaoishi Mjini wanapata huduma ya maji safi na salama sawa na 75%, uendeshaji wa mradi upo chini ya Bodi ya Mamlaka ya Maji Mjini. Aidha Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira bado ipo katika kundi C. Kutokana na ongezeko la watu kwa eneo la Mpwapwa mjini bado inawekwa mikakati ya upanuzi wa mradi ili uweze kazalisha maji kwa kutosheleza mahitaji wananchi. Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini mpwapwa inakabiliwa na changamoto zifuatazo;

- Upungufu wa watumishi wenyewe taaluma ya kuendesha mamlaka ya maji
- Madeni makubwa ya Ankara za maji za taasisi za serikali ambazo hazilipi bili za maji na kufanya deni kufikia zaidi ya Shilingi. 209,561,460.00 jambo ambalo limeisababishia Mamlaka kushindwa kulipa deni la Shilingi. 66,068,300 linalodaiwa na TANESCO
- Visima vya maji kuwekewa umeme wa LUKU

17.0 MKAKATI WA UANZISHWAJI WA VIWANDA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

Katika kutekeleza mpango wa kutenga maeneo ya viwanda, Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa imeweka mikakati ifuatayo:

- i. Kuandaa Mpango wa Jumla (Master Plan) unaoongoza upangaji na mwelekeo wa ukuwaji wa Mji wa Mpwapwa ambao utajumuisha matumizi ya uwekezaji na Viwanda.
- ii. Kutambua, kutwaa, kupanga na kupima maeneo mapya ya uwekezaji yanayofaa kwa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa.
- iii. Kuunganisha taratibu za ukuwaji wa mji, upangaji na mpango Mkakati wa uendelezaji wa miundombinu.
- iv. Kuhakikisha kila mchoro wa mipangomiji unaoandaliwa katika maeneo ya mji wa Mpwapwa na mji mdogo wa Kibakwe, unahusisha maeneo ya viwanda vidovidogo, vya kati na vikubwa.
- v. Kuhakikisha kila Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Vijiji unapoandaliwa unajumuisha matumizi ya ardhi ya uwekezaji wa viwanda.
- vi. Kushirikiana na wadau mbalimbali kuandaa Mpango Mkakati wa Utekelezaji na uwekezaji wa Viwanda katika Wilaya ya Mpwapwa.

- vii. Kukamilisha mchakato wa kutangaza katika Gazeti la Serikali maeneo yaliyokidhi vigezo vya kuwa miji, ili pamoja na matumizi mengine yapangwe matumizi ya viwanda. Maeneo hayo yanajumisha Kata ya Chipogoro, Mtera, Pwaga na Berege.

Sehemu B: Takwimu muhimu kwa ajili ya maeneo ya viwanda/Uwekezaji

Na	Eneo lililotengwa	Na. ya Usajili wa mchoro wa Mipangomiji	Ukubwa wa eneo	Idadi ya viwanja	Matumizi kwa sasa	Maelezo
1	Ilolo	-	3.7 Ha	40	Viwanda vidogo	Kati ya viwanja 40 Viwanja 3 vimeandaliwa Hatimiliki na 37 vinamilikiwa kwa Barua za Toleo.
2	Ilolo Mbuyuni	Mchoro wa Mipango Miji Na. 08/MPW/06/220 17	Eneo lililotengwa matumizi ya viwanda ni Hekta 1669, kati ya hilo ambalo lipo kwenye Mpango wa Matumizi (Proposed TP Drawings) ni Hekta 173.5		Eneo linatumika kwa matumizi ya kilimo (Mashamba) kwa vile taratibu za utwaaji wa ardhi (fidia) bado hazijafanyika,	Mpango wa ulipaji fidia umepangwa kutekelezwa mwaka wa fedha 2017/2018 JUMLA YA Shilingi 72,000= zimetengwa kuwezesha malipo ya fidia.
3	Visele	Mchoro wa Mipango Miji Na. 08/MPW/07/022 017	Eneo lililotengwa lina ukubwa wa hekta 27 na linatarajiwa kupimwa viwanja vya matumizi ya viwanda vya huduma (service industry)		Eneo linatumika kwa matumizi ya kilimo (Mashamba) kwa vile taratibu za utwaaji wa ardhi (fidia) bado hazijafanyika.	

4	Mji mdogo wa Kibakwe		Eneo lilitengwa lina ukubwa wa Hekta 6.6 kati ya hizo Hekta 4.5 zimetengwa matumizi ya viwanda nya kati na hekta 2.1 vimetengwa matumizi ya viwanda nya huduma. (Service industry)	Viwanja vilivyopendek ezwa kupimwa kupitia mchoro wa Mipango Miji ulioandaliwa ni 390.	Eneo linatumika kwa matumizi ya kilimo (Mashamba) kwa vile taratibu za utwaaji wa ardhi (fidia) bado hazijafanyika.	
---	----------------------	--	--	--	---	--

Hitimisho;

Baada ya kusema hayo, nakukaribisha tena Wilayani kwetu ili uendelee kutupa ushauri na kutuelekeza zaidi kwa nia ya kujenga Taifa letu

**JABIR M. SHEIKMWELI
 MKUU WA WILAYA
 MPWAPWA**